BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Sita – Tarehe 22 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

103. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Changamoto ya kuingiza mizigo kupitia Bandari ya Dar es Salaam inaendelea pamoja na juhudi kubwa iliyofanywa na timu ya utatuzi wa Kero za Muuungano inayoshirikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

(a) Je, Serikali inatambua kwamba bado waingizaji wa mizigo kutokea Zanzibar wanapata usumbufu mkubwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

(b) Je, ni sababu gani ya msingi inayowafanya wajasiriamali wadogo wadogo kutozwa fedha mara mbili wanapofika bandari ya Dar es Salaam pamoja na kuonyesha risiti za manunuzi kutoka Zanzibar.

(c) Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kulitatua tatizo hili na kero za Muungano zinazoendelea.

## Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

176. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Ni ipi njia mbadala ya kuwasaidia wananchi wa kisiwa cha Uzi ili waondokane na suala zima la uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na kukata mikoko na kuni kwa ajili ya kuuza na kupikia.

## Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

166. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ni kwa kiasi gani teknolojia inachangia urahisi wa kupatikana haki katika mahakama zetu kwa wananchi mbali mbali ikiwa ni pamoja na makundi maalum ya wananchi hao.

## Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

96. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Usalama na afya mahali pa kazi ni moja ya takwa la kisheria linalolenga kuhakikisha wafanyakazi wanatekeleza majukumu yao katika mazingira salama. Hata hivyo, suala la usalama na afya kazini limekuwa na changamoto kubwa Zanzibar, na hivyo kusababisha ofisi nyingi za umma na binafsi kutokukidhi vigezo vya usalama na afya kazini.

(a) Je, ni upi wajibu wa Idara ya Usalama na Afya kazini katika ukaguzi wa ofisi za umma ili kuhakikisha kuwa zinakidhi matakwa ya kisheria.

(b) Je, ni taasisi ngapi za Serikali zimekaguliwa tokea kuanzishwa kwa Idara hii na hatua gani zimewahi kutolewa kwa taasisi ambazo zinakiuka sheria na masharti ya usalama na afya kazini.

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi yanazingatia viwango vya usalama na afya kwa wafanyakazi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

183. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Licha ya Serikali kujitahidi katika kuwapatia vijana miradi mbali mbali, mingi ya miradi hiyo haiwi endelevu na mengine inaishia kushinda njiani.

(a) Je, Wizara imefanya tathmini yoyote juu ya uelewa wa changamoto hii.

(b) Ni aina gani ya miradi yenye tija na muelekeo wa kuwa endelevu ambayo Wizara yako imeiandaa kwa vijana kwa lengo la kuwapa muelekeo mpya wa mafanikio yao.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

179. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Miongoni mwa mabadiliko makubwa na ya kasi sana ya dunia, ni pamoja na kuelekea kwa kasi sana katika mfumo wa elimu mtandao.

Nini matarajio ya Wizara yako katika kukabiliana na mabadiliko ya mfumo mtandao katika mabadiliko ya kielimu hapa Zanzibar.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

69. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Je, ni upi mpango mkakati wa Serikali juu ya vijana wanaoranda ufukweni, kando ya mahoteli na kuwaibia watalii.

## Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

61. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Je, ni lini Serikali itatengeneza magari ya kuvunia mpunga ili wakulima wa Wilaya ya Kati waweze kufaidika na huduma hiyo.

242. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

    Ni lini Serikali itajenga machinjio makubwa yenye viwango na ubora unaostahiki.

## Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

35. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

    Tumekuwa tukishuhudia vitendo vya udhalilishaji kwa kina mama na watoto wadogo wa kike na kiume vikiendelea kwa kasi na kuporomoka kwa maadili kwa kiwango kikubwa nchini mwetu.

    (a) Je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha suala la udhalilishaji linakwisha.

    (b) Kwa kuwa kuna wazee na walezi ambao huitwa kutoa ushahidi na hawaitikii wito huo, Je, hatua gani Wizara inazichukuwa dhidi yao.

## Wizara ya Afya:

191. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Hivi karibuni kumeibuka taasisi na wafadhili mbali mbali wanaosaidia upatikanaji wa taulo za kike katika mashule yetu.

    Ni kwa kiasi gani Wizara ya Afya inasimamia udhibiti na ubora wa taulo hizo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

10. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    (a) Ni maeneo gani ambayo kwa sasa yananufaika na mawasiliano ya 5G hapa Zanzibar.

    (b) Ni yepi matarajio ya Serikali katika kuziunganisha taasisi zake kwenye mfumo mmoja wa mawasiliano ili kurahisisha utendaji wa shughuli mbali mbali za Serikali kwa kasi na uweledi zaidi.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**22 Mei, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**